# Njia NILIZOPITA

**Shikilia Maono Yako, Amini Mchakato, Furahia Hatima Yako**




**LIVINGSTONE ANDERSON MUSA**

# NJIA NILIZOPITA

*Shikilia Maono Yako, Amini Mchakato,*

*Furahia Hatima Yako*

LIVINGSTONE ANDERSON MUSA

Shikilia Maono Yako, Amini Mchakato, Furahia Hatima Yako

© 2024
**LIVINGSTONE ANDERSON MUSA**

**Mawasiliano:**

Kawaida: 0782 639 761.
WhatsApp: 0715 374 445.
Email: livingstonemusa761@gmail.com
Facebook: SUPERSTONE CHIDEBE II
Instagram: Superstone95
Tiktok: Superstone 99

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA!**

*Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya mmiliki wa kitabu hiki, isipokuwa kwa kunukuu kuliko ruhusiwa kisheria.*

ISBN: 978-9912-42-292-6

**Cover Design Na Typesetting imefanywa Vizuri Na:**
Lamax Designs, +255 764 793 105
lamaxdesigns@gmail.com
*(Nawe leta kitabu chako tukupangie)*

# YALIYOMO

UTANGULIZI ---------------------------------------------------------- x

Sura Ya Kwanza: KUZALIWA NA SAFARI YA ELIMU --------- 1

Sura Ya Pili: SIMBA KATIKA MSITU MZITO ------------------ 12

Sura Ya Tatu: MAISHA KATIKATI YA MSITU WA KOBOKO 37

Sura Ya Nne: JIJI LA KIBIASHARA KWA MARA YA KWANZA ------------------------------------------------------------------------ 61

Sura Ya Tano: SHAHADA NA CHUO BORA KWANGU ------ 75

Sura Ya Sita: NAIPENDA JAMII YANGU------------------------ 92

HITIMISHO--------------------------------------------------------- 116

MAREJEO --------------------------------------------------------- 119

# UTANGULIZI

*NJIA NILIZOPITIA: Ni kitabu kinachoelezea historia halisi ya maisha yangu hasa safari nzima ya kielimu toka ngazi ya chini hadi ya juu sana.*

Ni ukweli usiopingika kwamba kila mmoja ana njia yake ambayo anatakiwa kuipita ili kufikia hatima nzuri endapo tu atafanikiwa kuigundua njia hiyo au njia hizo. Katika hili wengi wamejikuta wakilazimisha kupita njia za wengine ambazo sio zao na matokeo yake wameishia kujikuta wakiweka akili na jitihada nyingi lakini matokea yake ni kukatisha tamaa, kitabu cha Joel Nanauka ***(CORE GENIUS),*** kinaweza kikawa msaada kujua njia yako sahihi ni ipi.

Kwa kiasi kikubwa nimekuwa mbishi kuamini kushindwa jambo kutokana na mtu fulani alishindwa (unaacha kitu kwa historia ya mtu mwingine) kwani nikiwa na miaka sita niling'ang'ania kuanza shule wakati wazazi wangu wakinikataza kwamba bado mdogo, nikiwa na miaka saba niling'ang'ania kwenda kuutafuta ukubwa (jando) wakati ambao wazazi wangu waliamini mwaka unaofuata ndio ungekuwa sahihi kwao, nikiwa kidato cha tano nilichukua maamuzi yaliyowaacha wanafunzi vinywa wazi kwa kujiunga na tahsusi ya HGL, iliyokuwa ikisadikika ni tahsusi ngumu sana pale shuleni kwetu na nikiwa mwaka wa kwanza chuoni licha ya kuwa na mazingira magumu

ya kiuchumi katika familia yangu, nilijiambia kwamba nitaacha utegemezi wa ada na hela ya matumizi toka kwa wazazi na nilifanikiwa.

CEO wa Ally Richy arts Ndugu Aliko Richard Mulungu aliwahi sema usiku mmoja wa hamasa ***"Mimi nikiamua jambo kwamba naliweza huwa sikatishwi tamaa hata aje nani, mpaka pale nitakaposhindwa mwenyewe ndipo nitakubali".***

Nimeandika kitabu hiki ikiwa ni sehemu ya kutimiza maono yangu ya miaka mitatu nyuma, kwani mwaka 2021 nilitaka kuandika kitabu kuhusu historia yangu, lakini nilipomshirikisha mwandishi mmoja wa vitabu aliniuliza swali hili, ***"Una nini haswa kikubwa cha kukufanya uandike kitabu cha historia yako?"***

Baada ya maneno yale sikukata tamaa nilianza kuandika kitabu lakini baadae nikaona ni kweli bado hakijitoshelezi nikaacha. Lakini pili, nimeandika kitabu hiki nikiamini kupitia maisha yangu na stori hii kuna watu wataenda kusaidika kwa namna moja ama nyingine.

***"Kitu anachokifanya mwanadamu ni matokeo ya yale yote ambayo aliyaona, kusikia, kunusa, kuhisi au kuyasoma katika kipindi cha nyuma"*** aliandika mwl. Joseph Mahindoni katika kitabu chake cha **SAFARI YANGU HATIMA YANGU.**

NJIA NILIZOPITIA: kimebeba mazingira ya ngazi mbali mbali pamoja na baadhi ya changamoto ambazo

nimezipitia, pengine ni changamoto ambazo nawewe unazipitia, utazipitia au mtu yeyote unamfahamu anazipitia, kupitia kitabu hiki anaweza kubadilika na kujiona mshindi kila wakati.

***Sala:*** *Eeh Mwenyezi Mungu Baba wa mbinguni, naomba umpe kibali huyu msomaji wa kitabu hiki aweze kupata nguvu na utulivu wa kukisoma, kutafakari na kupata majibu ya yale anayokutana nayo, anayotamani kufanya, apate uthubutu wa anayotamani kushinda na anatamani kuwagusa wengine kupitia maisha yake ya hapa duniani, Amen.*

***Get bigger than your challenge.***



*Picha ya pamoja na **Irene Ernest** wakati wa kusoma Risala ya wahitimu kwa mgeni rasmi **Mh. Diwani Andrew Mseya 2018.***

Isivyo bahati, kwenye ile ahadi nilipeleza pointi chache, hivyo ahadi ikawa imepotea japo kulingana na ugumu uliokuwepo pale nilijitahidi kuwasiliana na mh Diwani angalau anisaidie hata kidogo kwani nilikuwa nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Msakwalo iliyopo wilaya ya Chemba mkoa wa Dodoma.

Katika kipindi chote cha masomo wakati mzuri wakuwa na furaha ulikuwa ni ule nikiwa shuleni kuliko nikiwa nyumbani kwa wazazi, hata nyakati za likizo au kurudi kuchukua mahitaji nyumbani furaha yangu ilikuwa inadumu kwa siku chache za awali pale ninapofika

nyumbani na inapofika wakati wa kuondoka nyuso za huzuni zilitawala mara nyingi kwa wazazi wangu kwani walipenda sana waweze kunitimizia yale mahitaji muhimu kwa wakati lakini haikuwa hivyo, hali iliyopelekea migongano ya kifamilia wakati mwingine, hata mimi mwenyewe uso ulikosa nuru na kutamani kwenda shule hata kama sina mahitaji kwani nilipenda kuwaona wazazi wangu wakiwa na furaha.

## MAGEUZI YA USIMAMIZI WA BIASHARA

Mzee wangu alikuwa anamiliki genge lake la mda mrefu, ambalo kwa wengi lilionekana halikui miaka nenda rudi na kumbe ndicho kilikuwa kitovu cha kutusomeshea sisi kwani mimi na ndugu zangu tulipokuwa wadogo kila tukitoka shule au mzee akiwa hayupo basi mtoto mkubwa kwa wakati ule aliyekuwa nyumbani alihusika kwenda kuuza hasa nyakati za jioni, na hapa kila mtoto alipita kwa nyakati tofauti.

Hivyo, baada ya kuhitimu kidato cha nne 2018 nikashikilia usukani pale, nikawa nasimamia genge ili niweze kupata na fedha itakayonisaidia mahitaji ya kidato cha tano kule wilaya ya Chemba.

Sambamba na hayo niligundua umuhimu wa kuwa na vyanzo vya mapato zaidi ya kimoja ili chanzo A kinaposhindikana unatumia chanzo B, jambo halikuwa hivyo kwa familia yetu.